# Gazeti la Kimataifa

## Waabuduo Damu ya Kristo

...Kwa Neno Lako...

Lima, Peru
5–28 Luglio 2017

Mwaka XXI – N. 11, Disemba 2019

ASC Mawasiliano ya Kimataifa – Uongozi Mkuu - Via Maria De Mattias, 10 - 00183 Roma

www.adoratrici-asc.org redazioneasc@adoratrici-asc.org


Mhariri

## *Mawasiliano ni utume*

Mawasiliano maana yake ni kuingia katika mahusiano, na leo tunashukuru kwa uwepo wa vyombo vingi vya habari, tunaweza kuyafanya kwa namna mbalimbali, tukitumia zana mbalimbali za teknolojia zinazopatikana. Kuelezea mawasiliano kama utume, kwa vyovyote kunahitajika hatua zaidi, kwa kuwa yenyewe siyo tu fursa iliyobaki katika uhuru wa mtu binafsi au zawadi yake, bali yanawasilishwa kama wajibu, wito wa kuingia kwenye ulimwengu unaotuzunguka.

Kama hati ya Kanisa (Redemptoris Missio) inavyosema, ulimwengu wa mawasiliano unawakilisha Areopago mpya ya kuinjilishwa. Kwa kweli, siyo tu chombo cha kueneza Injili, bali pia ni sauti halisi ya lugha ya injili. Hata kama tunahisi usumbufu wa hitaji la kusukuma mbele teknolojia ambayo inatufanya kila wakati kwenda na nyakati, hatuwezi kuruhusu usumbufu huo kuhalalisha utendaji wetu, kwa maana Neno la Mungu ni hai kila siku ya historia, hapa na sasa, likituita tuwe Uwepo.

Uwepo ambao tunazungumza siyo uwepo wowote tu, na siyo moja ya uwepo wa aina nyingi ambazo zinapendekezwa kwetu. Hapana, ni UWEPO ambao unazungumza, unaofungua moyo kuwa na tumaini, unaoruhusu NJIA kutambuliwa miongoni mwa njia nyingi, njia ambayo haivutii kwa ahadi rahisi za kudanganya, isiyoahidi paradisi duniani, bali inatufundisha kuishi hali halisi ya kila siku.

Kwa hakika, Yesu Kristo alishuhudia kwetu, kwanza kwa umwilisho wake na kisha kwa Ukombozi, kwamba hatuko peke yetu katika safari yetu ya maisha. Anatembea pamoja nasi kando ya barabara za historia, huko Areopago, sehemu za mkutano ambapo watu hukutana, kufikiri, kuchagua, kuishi na kuteseka leo. Wakati Kristo anatembea pamoja nasi, tunaamini tumeitwa kukutana naye na kugundua uso wake ndani ya kila mtu na kila tukio, hata ikiwa ni tovuti, ukurasa wa Facebook, nk.

Nafasi ya vyombo vya habari ni taswira, lakini mahali pa kweli pa kukaa. Changamoto ni ile ya kuwa wazi kwa ulimwengu huu na kujifunza kuhusiana nao, kuleta na kuishi tunu za Injili, siyo kwa njia isiyofaa, bali kama raia ambao tunaishi historia yetu.

Kwa hivyo, teknolojia ni ishara ya hekima ya kimungu, ambayo Mungu anashirikisha kwa wanadamu bila hofu. Kwa hivyo, utume wetu ni ule wa kuweka mawasiliano ya kiteknolojia katika huduma ya ukuaji wa kiutu na wa kiroho.

***Sr. Maria Grazia Boccamazzo, ASC***

## Muhtasari


*Mhariri*
- Mawasiliano ni utume 1

*Nafasi kwa Uongozi Mkuu*
- Kupenda Mawasiliano 2
- Aima – Damu 3

*Toka Ulimwengu ASC*
- Sasisho toka Liberia 4
- Shukrani kwa jubilei ya Miaka 50 ya uwepo wa Waabuduo, Tanzania 5
- Tutawashukuru wale tunaowahudumia 6
- Kumshirikisha Maria De Mattias kwa Waseminari wa Damu Azizi 6
- Siku ya Misioni Duniani… 7
- Divai mpya … katika viriba vipya 8
- Mungu wangu – mpendwa wangu 9

*Nafsi kwa JPIC/VIVAT*
- Swachh Bharat Abhiyan 10

*Ndani ya Shirika*
- Kalenda ya Uongozi Mkuu 11
- Sikukuu za kuzaliwa: tusherehekee maisha 11
- Mikutano ya Region 11
- Waliorudi Nyumbani kwa Baba 11

# Kupenda Mawasiliano

*Kupenda Mawasiliano* ilikuwa ni mada ya semina iliyoandaliwa na UISG huko Roma Oktoba 17-19, ambayo niliihudhuria.

Mzungumzaji, Sr. Annmarie Sanders, IHM na mkurugenzi wa LCWR (Leadership Conference of Women Religious) aliwasilisha mawasiliano kama utume katika leo ya historia.

Bila shaka, wakati ambao tunaishi, mara nyingi mawasiliano hufafanuliwa kama jambo hatari na la utata, na yanapozungumzia maisha ya kitawa na tunu zake kwa kuyaweka katika utata. Walakini, tunashukuru kwa uwepo wa vyombo vya mawasiliano kwani watawa wana fursa ya kuwapo katika ulimwengu kwa njia tofauti, yenye ufanisi zaidi, wakijionesha wenyewe kama wale waliochagua njia nyingine ya maisha ambayo ni njia mpya ya kushuhudia tunu za Ukristo.

Bila shaka, kupitia vyombo vya habari, tunaitwa siyo tu kuzungumzia utume wetu, kile tunachofanya, lakini pia kiini cha maisha ya kitawa. Tunazungumza na kujitambulisha kuwa sisi ni nani, namna tunavyosali na kuishi na namna tunavyotafuta ustawi wa jirani na katika kila kitu kinachotuzunguka, namna tunavyoweza kusamehe, kile kinachotusaidia katika udhaifu wetu, tunalenga siyo tu katika kutenda, bali katika tunu na katika kiini cha maisha ya wakfu.

"Uwezo wa kusema, kuambiana kila mmoja, husaidia kuelewana na kuamsha tena siyo tu sehemu ya ufahamu bali pia hisia na mwili. Nafsi yetu hujibu kwa ujumla wake licha ya huruma au wema. Nani aliye bora kuliko watawa wanawake wenye masimulizi mengi ya kusimulia jinsi karama inavyomwilishwa katika mazingira ya leo?"

"Sababu ya pili ya kuambiana kila mmoja ni ile ya kutafakari pamoja. Kama sehemu maalumu ya wanawake watawa ipo katika ulimwengu wa kidijitali, hii inakuwa ni dhahiri: kuwa sauti, sura, mlio na uso wa ule uzuri pekee unazaliwa katika sehemu zile ambapo kila mmoja anaona tu mateso na vurugu. Kuwa digitali, mtazamo wa kidigitali unaosimulia Habari Njema, kuwa mtandao unaosikiliza ili wengine waweseze kushirikisha. Ikiwa sisi wanawake tunatunza maisha, itakuwa desturi yetu kutunza kile kinatembea ndani ya wavu. Ni ukweli usiopingika, kuuishi katika mazingira mengine tu."

Kwa hivyo, mawasiliano ni njia madhubuti ya kujibu hitaji la kiroho la ulimwengu, hasa la Wakristo na ujana.


Ukweli huu unatupa changamoto kila mmoja wetu kuimarisha njia ya maisha yetu ya ndani na kufanya mabadiliko ya kweli kutoka kwenye maarifa ya ujuzi kwenda katika tafakari ya kina, ambayo inatufanya tuweze kusoma uwepo wa kile kilicho kikuu zaidi katika katika mazingira ya kawaida ili kukibadilisha kuwa cha ajabu. Katika hili ni kweli tunapata maana ya mawasiliano, kama utume. Semina hiyo ilitoa kazi kwa kusudi hili, ikituwezesha kufanya mazoezi mbalimbali ya mbinu za tafakari na njia za kuuliza maswali juu ya maswala muhimu ya maisha. Yalikuwa ni mang'amuzi yenye maana sana kwangu ambayo yalinipa fursa ya kuimarisha jukumu la kuwasiliana, lakini zaidi ya yote kujua jinsi ya kuwasiliana.

Kama Waabuduo, kwa namna gani tunataka kweli kuiishi nafasi hii? Ni taswira ipi ya kuacha katika ulimwengu leo ambayo inaweza kufaa kesho? Jibu lipo katika changamoto ambazo tumeitwa, ambapo ni, kuweka hazina wakati wa sasa, ili kuweza kuishi kutoka katika undani ili kutoa nje Ukweli ambao leo ni muhimu kuurithisha.

***Sr. Maria Grazia Boccamazzo, ASC***



# Aima – Damu



## *Damu ya Yesu inatusaidia kujenga mahusiano …*

Msemu huu unatufanya tuingie kwenye roho ya siku tuliyoiishi huko Bari Carbonara tarehe 13 mwezi Oktoba 2019 pamoja na walei, marafiki zetu na wanachama wa Damu ya Kristo kutoka sehemu nyingi za Italia kusini (Puglia, Calabria, Basilicata.)

Pamoja na Sr. Nadia, Mkuu wa Shirika, na Sr. Dani, Msahauri Mkuu, nilikuwa na furaha ya kukutana na watu 300 waliounganishwa na tasaufi ya Damu ya Kristo na kuongozwa na Waabuduo Damu ya Kristo na Wamisionari wa Damu Azizi.



Mada ya mkutano ilikuwa *Aima, katika njia za historia*. Ulifanywa katika roho ya tafakari, adhimisho na uwazi wa kindugu.

Sr. Francesca Palamà, ASC, na Padre Enzo Napoli, CPPS, kwa furaha na ari waliongoza siku kwa uchangamfu na kwa mada ambazo zilituingiza vizuri kwenye tasaufi ya Damu ili kuiishi katika mahusiano yetu ya kila siku.

Kweli ilikuwa inatoa hamasa kuona ukumbi uliojaa vijana na watu wazima wakizunguka "kalisi ya ushirika" na kushangaa umakini na ushiriki katika mpango uliogawanyika katika nyakati tofauti. Kulikuwa na dansi ya masifu, maelezo ya Padre Luifi Maria Epicoco kuhusu Damu ya Kristo, muziki *To the last Drop* "The company of Miracles" ulioongozwa na Gianluca, CPPS, na ushuhuda wa washiriki.



Katika muda wetu wa pamoja na wa mahusiano katika Damu ya Kristo tuliuishi kikamilifu kila mmoja na tulikuwa na muda wa Misa kwenye Kanisa Kuu la Mt. Nicolaus la Bari, iliyoongozwa na Padre Oliviero Magnone, CPPS.

Baada ya Misa kulikuwa na mchezo wa kikundi cha Umoja wa vijana wa Damu ya Kristo kutoka parokia ya Damu Azizi ya Bari, pamoja na kikundi cha ngoma cha parokia kinachoongozwa na mwalimu Katia Laguaragnella. Mashahidi wa upendo, Waabuduo waliouwawa huko Liberia 1992, walikuwa ni walengwa wa mada "Hadi tone la Mwisho."

Siku iliyotumika kwa namna hii ilitutajirisha na kutupa nguvu ya kuendelea na safari kwa ari kubwa na kwa hamu ya kuimarisha zaidi tasaufi yetu ya Damu ya Kristo katika mahusiano yetu.

***Sr. Matija Pavić, ASC***

**Eneo la Bara: Afrika**
**Misioni ya Liberia**

# Sasisho toka Liberia

Salamu kutoka kwa Sr. Zita na Sr. Therese kutoka Liberia siku ya Jumamosi yenye mvua sana (Septemba 28), pamoja na juma la mvua. Msimu wa mvua umechelewa lakini kiwango cha maji ni cha juu.

Ni kiwango kizuri cha maji lakini siyo kwa kucheza watoto au kwa ajili ya kuvuna mpunga ambao uko tayari.

Juma la mwisho la mwezi Agosti, walimu walikutana kwa juma moja kwa ajili ya mafunzo katika maandalizi ya mwaka mpya wa shule. Hii ilikuwa ni mara ya kwanza, kama kawaida kulikuwa na siku moja ya masaa manne. Zawadi kwa ushiriki wa kila siku ilikuwa ni mlo mwishoni.



Tathimini ilikuwa nzuri pakiwepo maombi ya kufanya hivi kila muhula. Baadhi ya walimu wana elimu ya sekondari na wanafundisha kadiri wao walivyofundishwa. Wiki ilipangwa iwe ya vitendo na iweze kusaidia kiujuzi zaidi. Kilichoandaliwa kiliwasilishwa na walimu wenye uzoefu zaidi wakijumuishwa viongozi: ratiba ya masomo (miongozo ya Liberia), majaribio, kupanga, miongozo ya darasa, uongozi na mipango ya masomo.

Sista Therese alitoa huduma kwenye tume ya mipango na kuongoza siku ya kwanza katika kuangalia maana ya elimu, lengo na maelezo ya lengo, na kutumia miongozo ya nchi na jimbo. Mwisho wa kufurahisha kwenye wiki ilikuwa ni kupokea maelezo ya lengo siku ya Ijumaa kwenye Shule ya Mt. Patick.

Mkuu wa shule aliteuliwa siku kumi kabla ya kuanza shule, padre ambaye amekuwa akifundisha sekondari lakini hakuwahi kuhudumu kama mkuu. Alimwomba Sr. Therese afundishe dini kwenye madarsa ya 8 na 9 katika wiki sita za kwanza hadi hapo atakapozoea majukumu yake. Sr. Therese anarudi kufundisha wanafunzi aliowafundisha mwaka uliopita. Padre anafanya kazi kwa makini ili kujenga mazingira ya kujifunza yasiyo na kelele na milio wakati wa masomo. Ni mabadiliko yanayosaidia na ni mapya

Sista Zita anaendelea na madarasa yake matatu ya ushonaji na natumia muda mwingine kufundisha maarifa ya uokaji kwa wanawake wanaotaka kuoka mikate. Katikati ya masomo, anakuwa na kazi ya kurekebisha au kushona mashati au blauzi ambazo ni sare ya shule na kazi zingine za kushona. Kwa upande mwingine wanafunzi wanafanya kazi kadhaa kwenye uwanja.

Sr. Therese anaendelea kufanya kazi ya kuifanya maktaba ifanye kazi tena kwani imepita miaka 25 tangu kazi yoyote halisi ndani yake ifanyike. Baadhi ya wanafunzi hutumwa kusaidia kama adhabu kwa wamekosa yao. Wanafuta vumbi na kukusanya vitabu vya kupanga, hii inokoa muda kwa Sr. Therese ambaye ameanza kuvipanga kwenye shelfu kwa kufuata madarasa, kwa ajili ya walimu wa masomo mbalimbali. Lengo pia ni kuwa na sehemu



ya kutumia kama maktaba kwa jamii ya Grand Cess.

Hali ya hewa ni ya utulivu na tunaifurahia sana. Kwa wenyeji ni ya baridi. Utaratibu wa maombi ya visa ya Amerika kwa ajili ya kijana mvulana uliopangwa kwa ajili ya kwenda kufanyiwa upasuaji wa kurekebisha mguu wake na baba yake haujaenda vizuri. Mwishowe tumeweza kupata nafasi ya mahojiano Novemba 27, lakini nafasi ya awali katika hospitali huko St. Louis ilikuwa Novemba 7. Kwa bahati nzuri, tuliweza kubadilisha nafasi hadi Februari 6. Tunaombamsali ili visa itolewe.

Tunaendelea kukutana katika sala toka mbali .

***Sr. Therese Wetta, ASC***

# Shukrani kwa jubilee ya miaka 50 ya uwepo wa ASC, Tanzania

Tarehe 21 Septemba 2019, Ilikuwa ni furaha kubwa kwetu Masista ASC, Tanzania, kusherehekea miaka 50 (1969 – 2019) ya uwepo wa Shirika letu Tanzania. Maandalizi ya kusherehekea tukio hili muhimu yalianza kwa kusali sala maalumu kila siku, semina kutoka kwa Uongozi wa CIS, ziara mbalimbali zilizofanywa na jumuiya zetu kwenye makundi mbalimbali yenye jina la Mt. Maria De Mattias, Parokia na vigango, maandalizi ya kijumuiya na kibinafsi na hatimaye sala ya siku tatu. Ulikuwa ni muda mwafaka wa "kutafakari pamoja yaliyopita kwa moyo wa shukrani, kuyaishi ya sasa kwa moyo wa hamasa na kuyakumbatia ya mbeleni kwa moyo wa matumaini." Tulipenda kuwashirikisha wote si tu tukio hili bali pia upendo wa Mungu ambao katika miaka hii hamsini umedhihirika kupitia maisha na utume wa Masista Waabuduo, Tanzania, tangu dada zetu wanne Wamisionari wa kwanza Waabuduo kufika Tanzania (Sr. Angelina Palmigiani, Sr. Delfina Gnerre, Nicolina Scattaglia na Sr. Romana Sacchetti, ambao waliojitoa sadaka bila kujibakiza ili kuhakikisha kuwa upendo wa Mungu unaobubujika kutoka katika Damu Azizi ya Yesu unawafikia wote hasa maskini.



Tukio hili limetutia moyo na kutufanya kuwa na ari na moyo mkuu wa kusonga mbele ili kuendeleza karama ya Mt. Maria De Mattias na utume ulioanzishwa na masista wetu wanne sanjari na kuendelea kusoma alama za nyakati ili kusikiliza kwa makini na hatimaye, kujibu kilio cha maskini na wale wote wanaosukumizwa pembezoni mwa jamii. Limetuhimiza kutambua dhamana na wajibu wetu wa kujitakatifuza, ili kuweza kuwa mashuhuda wa Damu ya Agano Jipya na la milele, Fumbo la upendo, huruma na msamaha wa Mungu.

Katika ibada ya Misa Takatifu ya Jubilei iliyoongozwa na Mhashamu Baba Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya wakiwemo mapadre wengi, walishiriki watu wengi sana takribani elfu moja kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania. Askofu alisisitiza kuendelea kumwenzi Mt. Maria De Mattias. Alikazia malezi kwa vijana na watoto kuanzia ngazi ya familia na kila mahali, sote tuwajibike vema katika malezi ili Mungu aweze kupewa nafasi ya kwanza katika maisha yetu, na si vitu, maana vitu haviwezi kutupa furaha ya kweli ambayo Mt. Maria De Mattias aliihubiri.

Tunawashukuru Uongozi Mkuu wa Shirika letu na wanashirika wote kwa ushiriki na sala zenu. Mungu aendelee kutubariki ili katika Shirika hili, watu waweze kupata "misaada nyakati zote na mahali popote."

***Sr. Magdalena George Chipanta, ASC***

**Eneo la Bara: Amerika**
**Foundation ya Bolivia**

# Tutawashukuru wale tunaowahudumia

Karama ya Mtakatifu Maria De Mattias imeleta matunda katika nchi ya Bolivia. Kila Sista, Mwabuduo Damu ya Kristo alitoa maisha yake kwa furaha, akionesha huruma ya Yesu kwa wote walio masikini sana kwa utume wao wa afya, kuwatunza wasichana walio katika mazingira magumu, familia za vijijini na katika vituo vya elimu, pamoja na katekesi kwa watoto, vijana, watu wazima na familia, pia katika makazi duni, kwenye makanisa na parokia zilizo na malezi ya tasaufi ya Damu ya Kristo.

Tunafanya utume wetu wa elimu kwenye shule kwa watoto na vijana kwa kushudia imani yetu ya kikristo. Kituo cha pamoja cha Damu ya Kristo kwa ajili ya matunzo huduma za afya kwa watoto kupitia mpango wa msaada wa shule, mpango kwa ajili ya wazee na kituo kwa ajili ya kuwarudishia heshima watoto hasa wenye mahitaji ya pekee.

Kazi zingine za kitume tunazozifanya ni: hutuma za kijamii, chakula kwa ajili ya watoto, vijana na wasio na makazi, na utume kwa vijana kwenye maeneo ya vijijini.

Tunashirikishana na walei maisha na utume wa Damu ya Kristo.

Kwa kweli, Bolivia iko katika wakati mgumu wa hali ya kisiasa. Kwa sababu hii, tunawaalika kuendelea kueneza tasaufi ya Damu ya Kristo kama ishara ya upatanisho ili kujenga tena amani katika nchi yetu.

***Masista ASC wa Foundation ya Bolivian***



**Region ya USA**

# Kumshirikisha Maria De Mattias kwa Waseminari wa Damu Azizi




Vijana wa Damu Azizi huko Amerika Latin ambao wanajiandaa kwa ajili ya upadrisho wanaendelea na malezi katika mwaka wa mafunzo, sala na shughuli za kimisionari. Mwaka huu vijana watano katika malezi maalumu, wako hapa Guatemala. Wawili wanatoka Columbia, mmoja ni kutoka Peru na wawili kutoka Guatemala. Mlezi wao aliniomba kuwapa mafundisho ya siku kuhusu Maria De Mattias na tasaufi yetu.

Niliwaita baadhi ya masista wetu, Mary Kevin Rooney, Joan Hornick na Maria Hughes kushirikisha mawazo yoyote ambayo wangeweza kutoa. Sr. Mary Kelvin alikuwa na somo kamili ambapo alinifanya nifikiri kuwa angeweza kuja, na mimi ningeweza kuwa mkalimani wake. Lakini muda ulikuwa ni mfupi! Nilikuwa na matarajio kuwa huenda pakawa na fursa nyingine.

Mapatano pekee ambayo niliyafanya kabla, ilikuwa kwamba kutakuwa na sehemu ya huduma. Mtakatifu Maria alimkumbatia "jirani mpendwa" na tasaufi yake ambayo inatiririka kupita sisi katika ulimwengu wa leo, inajidhihirisha yenyewe katika uwepo wa huruma, kwa namna ya pekee miongoni mwa walio wahitaji zaidi. Nilitaka waalimu na wanafunzi katika Taasisi ya Maria De Mattias wawe na mang'amuzi ya "makuhani na makuhani wa siku zijazo" kama watumishi, wanaume ambao wanasimama pamoja na watu wa Mungu na wanaojitambua wenyewe kuwa ni wamoja pamoja nao. Na kwa hivyo baada ya asubuhi kamili ya mafundisho, mashirikisho, sala na tafakari, tulitumia muda wa mchana kwa kuchora, kupanda, kujenga na kuzungushia ua kwenye miti.

Hivyo, kwa matumaini, tulipokuwa tukijenga na kupendezesha, roho ya Maria ilipanda hamu ndani yao ili kutafuta njia za kuwa katika huo "mpango mzuri." Na kama wengi wetu tunavyojua, kusali, kupanga na maandalizi ya siku yalikuwa zawadi ya kweli.

***Sr. Kris Schrader, ASC***

# Siku ya Misioni Duniani …

Siku ya Jumapili, Oktoba 20, 2019, wakati Kanisa lilipokuwa likisherehekea Siku ya Misioni Duniani, tulianza rasmi utume wetu katika jimbo la Teggiano-Polcastro. Tunakaa katika Bellosguardo, mji mdogo wa urefu wa mita 500 katika milima ya Alburni, katika hifadhi ya kitaifa ya Cilento na Vallo di Diano, lakini pia tunatoa hudumua huko Roscigno mji mwingine wa karibu.

Wakati Askofu Giuseppe De Luca alipokuja kutembelea kitambo kabla ya adhimisho Misa ya kukaribishwa, alituarifu kwamba hivi karibuni mradi wa elimu kuelekea makaribisho utaanza hapa Bellosguardo. Mradi huu ulianza kama ushirikiano wa Jimbo na baraza la mji na Chuo Kikuu cha Posillipo. Askofu nataka sisi tushirikiane katika mradi huu pia, kwa kiwango ambacho kila mmoja anaweza kufanya hivyo. Kwa kweli, jamii mbili kubwa za wahamiaji wa Kiislamu wanaishi Bellosguardo na Ottati, mji ulio kwenye kilima kilicho mbele yetu. Miongoni mwa malengo ya mradi huo ni ule wa kukua katika ujuzi wa kupokeana na kuimarisha tunu za tamaduni nyingi.

Wakati huo huo, tunapojikuta bado tunashughulika katika kuandaa nyumba, tunaanza na vitu vidogo: kufanya manunuzi, kwenda Kanisani, kukutana na watu wanaokuja kutusaidia kupanga vitu. Hii yote ni fursa za kuanza kujenga mahusiano. Kushiriki katika mikutano ya utume na katekesi kunatuweka katika shughuli za kawaida za kazi za kichungaji na kutufanya tuonje uzuri wa kuishi katika mji mdogo.

Wiki moja tu baada ya kufika kwetu, kwa furaha na mshangao, tunakumbuka hatua kadhaa kabla ya kuja kwetu rasmi hapa.

Hatua ya kwanza ilikuwa Septemba 29, sikukuu ya Mtakatifu Michael Malaika Mkuu, mlinzi wa Bellosguardo. Tulishiriki sherehe kuu ya kufunga maadhimisho, mwishoni Padre Antonio Romaniello, alitutambulisha kwa waamini na kusema maneno machache ya kutukaribisha.

Asubuhi iliyofuata tulirudi Roma tukitamani kuanza njia hii mpya ya maisha haraka iwezekanavyo. Siku zilizofuata, Sr. Miriam De Michele na Sr. Milena Marangoni walihakikisha matayarisho ya nyumba yamekamilika na matarajio ya kuwasili kwetu, walikaa kwa muda huko Bellosguardo ili kuweka vitu vizuri kwa ajili yetu na kusafisha nyumba. Uwepo wa washauri wa Region ambao walikuja mjini kila mara kwa muda, uliamsha hamasa ya watu ambao, kwa kuona sura mpya, walishangaa ni nani hao watatu na ni nani watabaki. Jioni ya Oktoba 20 tulikuwa watu saba, watatu wa jumuiya hiyo waliosindikizwa na Sr. Milena, Sr. Miriam, Sr. Lucia resta na Sr. Bruna Menichelli. Askofu alikuja kutuchukua nyumbani na tukaenda kwenye kanisa la parokia pamoja na yeye na Padre Antonio ambapo watu wengi kutoka Bellosguardo na Roscigno walitukaribisha. Kati ya waadhimishaji wa Misa alikuwa Msgr. Orazio Pepe, Padre wa Jimbo mzaliwa wa Bellosguardo ambaye anafanya kazi huko Roma. alisisitiza kwamba tunadaiwa kufungua jumuiya. Miongoni mwa waamini walikuwepo viongozi wa serikali na wanafunzi wa shule ya msingi na walimu wao waliotukaribisha mwishoni mwa Misa. Watoto waliimba "Mbingu hazina mipaka," wimbo ambao unamwalika kila mtu kumkaribisha kila mtu kama ndugu. Sherehe ya makaribisho ilimalizika kwa chakula cha jioni uwanjani na kukata keki mpya ya makaribisho. Sasa tunahitaji na tunataka kuanza kwa unyenyekevu na uaminifu.



***Jumuiya ASC ya Bellosguardo***
***Sr. Patrizia Pasquini, Sr. Genesia Nave,***
***Sr. Maria Chiara Maselli***

# Divai mpya … katika viriba vipya

## *Pamoja katika safari ya sinodi*



***Kazi ya Carmela Boccasile***

Kikao cha kwanza cha mkutano wa IV wa Region ya Italia kilifanyika katika nyumba kuu ya Mapadre Wapasionisti huko Roma kuanzia Novemba 1 – 2, 2019. Wajumbe wa kuchaguliwa walishiriki, lakini kwa lengo la kuanza mchakato uliohusisha kadiri iwezekanavyo karibu masista mia nne wanaotoa uhai kwa Region ASC. .

Wazo msingi ni lile ya kufanya mchakato wa pamoja wenye imani mkubwa, ambalo, kwa kupitia kikao cha pamoja na kamali kilichofuata, lingeweza kutoa fursa kwa idadi kubwa ya masista kuchangia mawazo yao kikamilifu kwa ajili ya maisha yetu na utume wetu. Katika vikao kila mshiriki alikuwa na fursa ya kutoa mapendekezo yake, kushirikisha mawazo yake, na kupiga kura ya mapendekezo kuhusu mwelekeo wa kuchukua.

Mada iliyopendekezwa na Uongozi wa Region ilipata msukumo kutoka CICLSAL, hati iliyochapishwa kwa kibali cha Papa Franccis tarehe 6 Januari, 2017: Divai Mpya katika viriba vipya. Kwa hiyo, tunatafakati juu ya mada hii,

*Tumetengeneza divai mpya kutoka katika mavuno yetu ya zabibu?*
*Tumetoa viriba vipya vya divai? (Rej. Mk. 2:22)*
*Leo ya Familia yetu ASC*

Alama ambayo tulijisikia kuwakilishwa nayo ni picha ya mwanamke anayetazama anga angavu ambalo mwanga wake unamfanya asione vizuri, bila shaka tunajua kuwa tunaishi katika kipindi cha mabadiliko makubwa ambapo maisha ya wakfu, na sisi pamoja nayo, tunaonja kwa kina hali ya mfadhaiko na mashaka kuhusu wakati ujao, hata kama Mungu haachi kutuongoza kwa mwanga wake.

Walakini, kwa uhakika katika Bwana tunataka kujiuliza wenyewe 'sisi ni nani na tunataka kuwa nani' ili ushuhida wetu atufanye uwazi wa Kristo na kazi yetu katika shamba la mizabibu la Bwana izae divai mpya ya kutosha, ambayo Baba anaitaka.

Mchana wa siku ya kwanza ya kazi, baada ya utangulizi na sala nzuri ya ufunguzi wa Mkutano, Sr. Nicla Spezzati, Mkuu wa Region, aliwasilisha picha halisi ya ukweli wetu. Katika ripoti yake, Divai mpya: changamoto kubwa ya maisha ya wakfu leo, aliweka ukweli wetu kama Region ASC katika muktadha wa jamii na Kanisa la sasa, akituonesha nguvu zetu na udhaifu wetu.

Bila kukatishwa tamaa na shida hizo, alitutia moyo kuamini kuwa siku zijazo zinawezekana, lakini kwa njia tofauti na jinsi ambavyo tutakuwa tumeziota tangu leo. Alihitimisha kwa maneno maarufu ya kinabii ya Benedict XV, "Kanisa ambalo litakuwa limepoteza jamii litachipukia kwenye anguko la leo. Litakuwa dogo na litalazimika kuanza tena mwanzoni kabisa au mwanzoni kidogo toka mwanzo. Lakini, licha ya mabadiliko haya yote, Kanisa litapata kile kilicho muhimu kwake tena na kwa nguvu kubwa. (…) Mchakato utakuwa mrefu na wa uchovu. (…) Katika upweke wao usioweza kuelezeka, watu watagundua jumuiya ndogo ya waumini kama kitu kipya kabisa. Baadaye wataigundua kama tumaini lao, jibu ambalo wamekuwa wakilitafuta kwa siri (...) Kanisa litapata ustawi mpya."

Katika mashirikisho yaliyofuata wakati wa kazi kuzunguka meza mbali mbali, tafakari ilitokana na uzoefu wa imani na uzoefu wetu wa utume kibinafsi na kijumuiya. Yalituongoza kuainisha michakato kadhaa ya uvumbuzi ambayo tunaweza kuizingatia. Tuko tu mwanzoni mwa mchakato ambao sasa utahitaji kuchimbuliwa kwa kina katika mikutano ya pamoja na kushirikishwa na kila mmoja.

***Sr. Patrizia Pasquini, ASC***

# Mungu wangu – Mpendwa wangu



Mkusanyo wa mashairi wenye jina "Mungu Wangu - mpendwa wangu" ulichapishwa msimu huu wa masika huko Zagreb. Ni kazi ya Ana Marija Miskulin, mwanamke wa miaka 24 aliye na ugonjwa wa kupooza kwa ubongo.

Mkusanyo wa mashairi ulihaririwa na kuandaliwa kwa ajili ya kuchapishwa na Sista Tomislava Ćavar, profesa wa lugha ya Kikroesia na mkuu wa Kituo cha wahariri wa Region ya Zagreb. Utangulizi uliandikwa na Sista Cecilija Milković, mkurugenzi wa mpango wa Maria De Mattias Foundation, ulioandaa uwasilishaji wa kitabu hicho. Ubunifu na picha za kava zilifanywa na Petra Ćurković, ambaye ni mwanafunzi. Mradi wote ulifanywa kwa kushirikiana na Jumuiya ya ufadhili ya Ruah ya Samobor, ambayo inasaidia mikakati na mipango ya kusaidia watoto wenye ulemavu wa kudumu, shida na mahitaji maalum.

Miaka miwili iliyopita, mwishoni mwa mwaka wa 2017, Maria De Mattias Foundation iliwezesha kuchapishwa kwa ukusanyaji wa kwanza wa mashairi na maandishi ya kiroho ya Ana Marija, "ambayo pia yalisahihishwa na kutayarishwa kwa ajili ya kuchapishwa na Sr. Tomislava.

Uwasilishaji wa kitabu hiki ulikuwa tarehe 23 Septemba, 2019, katika ukumbi wa mkutano wa Waabuduo Damu ya Kristo kwenye nyumba ya Miramarska Zagreb. Marafiki wa chama cha Ruah na MDM Foundation walikuja kwenye hafla hiyo, pamoja na ASC wengi. Kikundi cha muziki cha Chama cha Ruah kilionyesha muziki na nyimbo ili kufanya wakati huu wa pamoja kuwa sherehe ya kweli ya urafiki na ya furaha.

Sr. Sunčica Kunić alikuwa mgeni rasmi wa sherehe za mpango huu. Katika kumtambulisha mwandishi, alisema, "Ana Marija ameandika maandishi ambayo yanaelezea ukuu na uzuri wa upendo wa Mungu. Yeye anaishi katika nyumba ya Mt. Vincent wa Paul nyumba ya Caritas huko Oborovo. Yeye mwenyewe alisema kuwa kwa kuwa tangu alipokutana na Bwana, kiti chake cha magurudumu kimekuwa baraka kwake na kwa nyumba ya Mt. Vincent mahali ambapo asingeweza kubadilishana na kitu chochote.

Akizungumza juu ya mkusanyo wa mashairi, Tomislav Šovagović, mwanateolojia, mwandishi na mtangazaji wa habari, alisema miongoni mwa mambo mengine, "Ana-Marija anajieleza mwenyewe kwa unyofu wa kitoto, ambao ni hitaji la shairi lolote. Akimzungumzia Mungu, mashairi yake ni sala na mkusanyo huu kweli ni kitabu kidogo cha sala. Kwa kumwongelea Mungu wakati wa ugonjwa, wasiwasi, na mateso ni ushuhuda mkubwa, lakini wakati hali hizi zikiwa ni za kudumu, kila siku, basi sala yake na ushairi viliimarika zaidi. (…) Hii ndio sababu mkusanyo wa "Mungu Wangu, mpendwa wangu" ni, wakati huo huo, mwaliko unaotolewa kwetu sote kuacha kulalamika na kulia, na hivyo basi kuelekeza maneno yetu Mbingu na siyo kuchelewa sana kwa sababu tunatajirisha ulimwengu, kama ulivyo mkusanyo wa pili wa mashairi ya Miskulin.

Kwa kurejelea kitabu hicho, Sr. Tomislava Ćavar anasema kwamba Mungu alimpa Ana Marija msalaba mgumu sana, ambao kwa kweli wengi wetu tungekimbia! Lakini Ana Marija anafanya kile ambacho kila mmoja wetu anapaswa kufanya katika mazingira magumu: anatafuta ufafanuzi na anauliza ni kwa nini, anagombana na Mungu, lakini hakimbii. Anakubali mateso na kujaribu kuyapa maana. "Ninamshukuru mwandishi kwa kushuhudia kwamba Mungu ndiye kila kitu kwake." Na alisisitiza, "Nunua kitabu na utafute neno la Mungu kwa ajili yako na Mungu aliye ndani yako.

Maneno ya mwandishi, yaliyotangazwa kwa shida na Ana Marija mwenyewe, yalikuwa ya motomoto na yalimgusa kwa ndani kila mtu aliyekuwepo. Kukutana kwetu na uinjilishaji wake, kunatia moyo, na mshangao. Alitoa shukrani zake kwa wale wote waliomuunga mkono na kufanikisha uchapishaji wa kitabu hicho. Mwishowe, kikundi cha muziki cha Ruah kiliimba wimbo "Mwenyezi Mungu," kwa kutumia maneno yaliyoandikwa na Ana Marija. Wasikilizaji walifurahia wimbo huo.

***Sr. Vesna Abramovic, ASC***

## Swachh Bharat Abhiyan








Swachh Bharat Abhiyan (SBA) ni kampeni ya kitaifa nchini India kwa kipindi cha 2014 - 2019, ambayo inakusudia kusafisha maeneo ya mitaa, barabara na miundombinu ya miji ya India, majiji, na vijiji. Jina rasmi la kampeni liko katika lugha ya Kihindi na hutafsiri hivi "Neat and tidy India Mission" kwa Kiingereza. Kampeni ilizinduliwa rasmi tarehe 2 Oktoba 2014 huko Rajghat, siku muhimu kwa Wahindi kwani ni Siku ya Kuzaliwa kwa Mahatma Gandhi na tarehe 2 Oktoba 2019 ni Sikukuu ya Kuzaliwa ya 150 ya Gandhiji.

Kwa kujiunga na kampeni hii, Shule ya Mt. Maria, Chund (Ranchi) imeandaa "Swachhata Abhiyan" Hifadhi ya Usafi pamoja na walimu na wanafunzi. Tulikuwa tumechagua kijiji kiitwacho Thakurgaon, kilomita chache kutoka shule yetu. Wanafunzi walifurahi sana na kushangilia na kutengeneza vipeperushi na mabango kwa kusudi hili. Walileta pia ufagio, koleo, mafyekeo, panga na n.k. kwa ajili ya kuvitumia kwa kazi hiyo. Tarehe 2 Oktoba 2019 ni siku ya kushangaza katika historia ya Shule ya Mt. Maria, Chund. Tulianza kutoka shuleni saa 9.00 asubuhi na kufika kijijini saa 9.20 asubuhi. Mwenyekiti wa kijiji cha Thakurgaon, polisi wawili na wazazi wachache waliowakilisha wazazi wote walikuwepo kutusaidia na kutuongoza.

Mwanzoni tulifanya gwaride lililoshikilia vipeperushi na mabango na kusoma matangazo ili kutoa uelewa kwa watu juu ya kutunza mazingira yao katika hali ya usafi. Baada ya hapo, wanafunzi waligawanywa katika vikundi vidogo na kuanza kusafisha barabara na mitaa kwa kuondoa taka za plastiki, majani makavu na kufagia barabara. Baadhi ya wakaazi na wafanyabiashara wa eneo hilo pia walijiunga nasi kwenye kazi hii ya usafi. Tulirudi shuleni saa 11.45 asubuhi.

Kwa kweli yalikuwa mafanikio makubwa. Wanafunzi walifurahi sana kuwa sehemu ya harakati hii kubwa na watu wa eneo hilo walithamini sana mpango huu kutoka shuleni. Ulikuwa ni uzoefu wa pekee kwetu sisi sote..



***Sr. Mini Vadakumpadan, ASC***





## Kalenda ya Uongozi Mkuu

**Disemba 4-10:** Sr. Maria Grazia Boccamazzo atakuwa Croasia kwa ajili ya kufanya kazi na katibu wa Region
**Disemba 5-22:** Sr. Nadia Coppa na Sr. Bridget Pulickakunnel watakuwa Tanzania kusindikiza Mkutano wa uchaguzi wa region
**Disemba 15 – Januari 11:** Sr. Manuela Nocco atakuwa Tanzania kwa ajili ya kufanya kazi na mhasibu wa Region
**Disemba 22:** Tamasha la nyimbo za Krismasi za mashirika Nyumba Kuu kwenye Kanisa la Damu Takatifu

## Sikukuu za Kuzaliwa: Tusherehekee maisha ya:



| | | |
|---|---|---|
| 30 | | |
| **Sr. Lazara Silva Indi** | 12/17/1989 | Guinea Bissau |
| 40 | | |
| **Sr. Mariana Wegoro Peter** | 18/12/1979 | Tanzania |
| 60 | | |
| **Sr. Maria Elena Bilbao** | 01/12/1959 | Italia |
| 70 | | |
| **Sr. Edita Janko** | 13/12/1949 | Zagreb |
| **Sr. Maria Mercedes Redondo Gutierrez** | 22/12/1949 | Hispania |
| 80 | | |
| **Sr. Antonietta Ciuffreda** | 16/12/1939 | Italia |
| **Sr. Esperanza Razura Villarreal** | 17/12/1939 | USA |
| **Sr. Rosa Pereira Teles** | 25/12/1939 | Manaus |
| **Sr. Maria Poppa** | 26/12/1939 | Italia |
| **Sr. Maria Caruso** | 28/12/1939 | Italia |
| 90 | | |
| **Sr. Lucia Pacifico** | 23/12/1929 | Italia |
| **Sr. Alba Falcone** | 28/12/1929 | Italia |
| 100 | | |
| **Sr. Bernice Taylor** | 25/12/1919 | USA |

## Mikutano ya Region

*Disemba 14- 18*

Mkutano wa uchaguzi **Tanzania**

## Waliorudi Nyumbani kwa Baba



| | | |
|---|---|---|
| 08/11/2019 | **Sr. Marianna Konefał** | Wrocław |
| 13/11/2019 | **Sr. Raffaella Colucci** | Italia |
| 16/11/2019 | **Sr. Michelina Miletti** | Italia |

**Gazeti la Kimataifa**
*Waabuduo Damu ya Kristo*
...Kwa Neno Lako...

**Habiri ya kila mwezi**
*na*
***Waabuduo Damu ya Kristo***
***Mawasiliano ya Kimataifa - Uongozi Mkuu***
Via Maria De Mattias, 10 - 00183 ROMA
**Mwaka XXI, N. 11, Disemba 2019**

*Kamati ya wahariri*
**Maria Grazia Boccamazzo, ASC**
**Debora Brunetti**

Tafsiri na
***Sr. Klementina Barbić*** *- Kikroeshia*
***Sr. Betty Adams*** *- Kiingereza*
***Sr. Martina Marco*** *- Kiswahili*
***Sr. Bozena Hulisz*** *- Kipolishi*
***Sr. Clara Albuquerque*** *- Kireno*
***Sr. Miriam Ortiz*** *- Kihispania*
***Sr. Johanna Rubin*** *- Kijerumani*